

Mafuriko - hatari za wanyama na wadudu

Habari juu ya jinsi ya kukabiliana na wanyama na wadudu kisha mafuriko

Swahili | Kiswahili

OFFICIAL

Unaporudia kwenye eneo iliogusiwa na mafuriko, wanyama wa porini, wakiwemo panya, nyoka au buibui, wanaweza kuwa wamenaswa nyumbani kwako, banda au bustani yako.

Kushughulika na nyoka

- Ukiwa nje ya nyumba:
 - ✓ vaa buti imara (bottes ya nguvu), glavu (gants) na suruali ndefu ili kulinda miguu yako
 - ✓ uwe makini zaidi kuhusu mikono na miguu yako wakati wa kusafisha kisha mafuriko
 - ✓ ukiona nyoka, rudi nyuma na uiruhusu iende kwenye njia yake - usiiguse
 - ✓ uwe makini na nyoka wanaoagelea ndani ya maji
 - ✓ unapaswa kuondoa uchafu unaozunguka nyumba yako kwa sababu unaweza kuvutia nyoka, buibui, na panya.
- Ikiwa unapata nyoka ndani ya nyumba yako, usiogope, rudi nyuma polepole kutoka kwake na uiruhusu kuendelea kwenye njia yake. Usiiguse Piga simu kwa Idara ya Mazingira, Ardhi, Maji na Mipango (Département ya Environnement, Terre, Eau et Plan) kwa nambari 136 186 ili kupata orodha (liste) ya wakamata nyoka katika eneo lako.
- Ikiwa unaumwa na nyoka:
 - ✓ usioshe ngozi karibu na sehemu uliyoumwa
 - ✓ tulia na pata usaidizi wa haraka wa matunzo kwa kupiga simu 000
 - ✓ lala chini au keti na kuumwa chini ya kiwango cha moyo wako (couchez-vous par terre ou asseyez-vous avec la morsure en dessous du niveau du coeur).
 - ✓ funika eneo hilo kwa nguo safi na ya kukauka. Ikiwa inapatikana, weka bandage kwa uimara karibu na eneo ambalo kuumwa kulitokea pia inashauriwa.
 - ✓ kumbuka wakati wa kuumwa na wakati bandage iliwekwa
 - ✓ usifunge kamba au bandege ya kukataza damu isitembeye katika mishipa, usikate sehemu iliyoumwa ili kutoa sumu au jaribu kunyonya sumu kutoka kwenye kidonda .

Kushughulika na buibui

- Ikiwa unaumwa na buibui:
 - ✓ osha eneo hilo na tumia vifurushi vya barafu kusaidia kupunguza maumivu
 - ✓ usifinye
 - ✓ tafuta usaidizi wa muganga moja kwa moja ikiwa uliumwa na buibui wekundu au dalili zako zikizidi kuwa mbaya.

Kukabiliana na panya na wadudu

- Wanyama kama vile panya pori na panya hubeba magonjwa. Unapaswa kuondoa chakula na vitu vingine ambavyo vinaweza kutoa makao kwa panya.
- Ondoa uchafu na weka kifuniko kwenye ngungulu ya uchafu. Weka mitego ya panya katika maeneo ya kukauka ikiwa inahitajika.
- Kaa mbali na maji yasiyo tingizika kwani imbu zinazaliana humo. Funika mwili wako kadri uwezavyo na tumia dawa ya kufukuza imbu.
- Inzi hubeba magonjwa. Safisha uchafu wa chakula mara moja kwani ni fasi ya kuzalia inzi.
- Iwapo utaumwa au kuumizwa na mnyama au kuumwa na wadudu pata ushauri kutoka kwa daktari wako au piga simu MUUGUZI – WA – ZAMU (INFIRMIER DE GARDE) saa 24 kwa siku, siku 7 kwa wiki kwa 1300 60 60 24.

Ili kupokea chapisho hili katika muundo (format) unaofikiwa, tuma email pph.communications@health.vic.gov.au

